TOLEO Na. 18 | OKTOBA 2024

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

JARIDA LA

# SAUTI YA JIJI

## TOLEO MAALUMU KUELEKEA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

## RAIS SAMIA AHIMIZA AMANI NA UTULIVU KATIKA ZOEZI LA UANDIKISHAJI NA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA 2024

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa Watanzania kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili waweze kutimiza haki yao.... **UK 1**




**JIANDAE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NOVEMBA 27, 2024.**

# RAIS SAMIA AHIMIZA AMANI NA UTULIVU KATIKA ZOEZI LA UANDIKISHAJI NA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

**Na** Shalua Mpanda

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa Watanzania kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili waweze kutimiza haki yao kikatiba ya kuwachagua viongozi wa Serikali za Mitaa katika maeneo wanapoishi.

Rais Dkt. Samia ametoa wito huo wakati akizindua rasmi zoezi la uandikishwaji kwenye daftari hilo lililofanyika Oktoba 11,2024 katika ofisi ya Serikali ya Mtaa wa Chamwino Ikulu, Kitongoji cha Sokoine.

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kujiandikisha katika kituo hicho, Rais Dkt. Samia amewapongeza kwa kujitokeza kwa wingi, pamoja na mambo mengine amewataka wananchi kushiriki zoezi hilo la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa amani na utulivu.

Zoezi hilo la Uandikishwaji katika Daftari la Mpiga Kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa lililochukua takribani siku 10 lilitamatika rasmi tarehe 20 Oktoba, 2024.

Aidha, kwa mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Sikukuu za Kitaifa (Public Holidays Act) Sura 35, Rais Dkt. Samia ametangaza tarehe 27 Novemba, 2024 kuwa siku ya mapumziko ili kuwaruhusu wananchi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.







> *"Tushiriki zoezi hili la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa amani na utulivu."*

# UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WAIVA: VIJIJI 12,333, VITONGOJI 64,274 NA MITAA 4,269 KUHUSIKA.

**Na** OR-Tamisemi

Mwaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa ametangaza jumla ya Vijiji 12,333, Mitaa 4,269 na Vitongoji 64,274 kuwa vitashiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, 2024.




Akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha Jumatatu Septemba 16, 2024 kwenye Ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Mchengerwa amewaambia wanahabari kuwa orodha hiyo imejumuisha maeneo yaliyokuwa yamefutwa awali kwa mujibu wa tangazo la serikali ambayo pia yalihusisha Tarafa ya Ngorongoro mkoani Arusha.

Mhe. Mchengerwa amesema Notisi ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Tangazo la Serikali namba 769 la mwaka 2024, limetolewa kwa mujibu wa vifungu vya 16(1) na 18(1) vya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288

Tangazo hilo limebainisha mipaka ya vijiji, mitaa na vitongoji vitakavyohusika katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024 na pia Tangazo hilo limerejesha vijiji vya Ngorongoro vilivyofutwa kwa tangazo la Serikali namba 673 na Tangazo la Serikali namba 674 la Agosti 02,2024.

Aidha Mhe. Mchengerwa amewataka Watanzania kujiorodhesha katika orodha ya wapiga kura kati ya Oktoba 11 hadi Oktoba 20,2024 na pia kujindaa katika kugombea nafasi mbalimbali za Uongozi katika uchaguzi utakaofanyika Novemba 27,2024.

'Ofisi ya Rais Tamisemi imejiandaa vyema kuhakikisha kwamba uchaguzi huu unakuwa huru na wa haki katika misingi ya 4R kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kusisitiza. Mchakato huu ni fursa kwa wananchi kushiriki moja kwa moja katika kuamua mustakabali wa maendeleo ya maeneo yao.´




KAULI MBIU:
**"SERIKALI ZA MITAA, SAUTI YA WANANCHI, JITOKEZE KUSHIRIKI UCHAGUZI."**

# MKURUGENZI WA JIJI LA DSM ATOA WITO KWA WANANCHI KUJIANDAA NA KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024




**Na** Judith Damas

Wito huo umetolewa Oktoba 2, 2024 na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam Ndugu Elihuruma Mabelya wakati akiongoza zoezi la utoaji wa elimu pamoja na kugawa vipeperushi kwa Wananchi, Wafanyabiashara pamoja na Watumishi mbalimbali kutoka ofisi za Mitaa na kata ya Jiji la DSM. Tukio hilo lililofanyika katika eneo la Kaburi moja Kata ya Mchafukoge lengo likiwa ni kuwafikia Wananchi na kuhakikisha wanatumia fursa hiyo katika kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ifikapo tarehe 11 hadi 20 Octoba 2024 kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe 27.11.2024.

Aidha Mkurugenzi Mabelya ameeleza kuwa Kauli mbiu ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa imelenga kuwakumbusha wananchi umuhimu wa Serikali za Mitaa hivyo wajitokeze kushiriki uchaguzi Ili waweze kuchagua viongozi bora kwa maendeleo ya Jiji na Taifa kwa ujumla.

Pia Mkurugenzi huyo ametumia fursa hiyo kusisitiza juu ya suala la amani na utulivu kuelekea uchaguzi huo ambao utatoa dira ya maendeleo katika Mitaa,Vitongoji na Vijiji hapa Nchini.






JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

OFISI YA RAIS TAMISEMI
JIANDIKISHE PIGA KURA
27 NOVEMBA 2024
UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA




KAULI MBIU: **"SERIKALI ZA MITAA, SAUTI YA WANANCHI, JITOKEZE KUSHIRIKI UCHAGUZI."**

**TUFUATILIE** SASA KUPITIA

jiji_la_dsm

# WASIMAMIZI WA UCHAGUZI JIJI LA DSM WATAKIWA KUFUATA MAELEKEZO NA SI KUFANYA KAZI KWA MAZOEA



**Na** Judith Damas

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Ndg. Elihuruma Mabelya amewataka wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kufuata maelekezo na sio kufanya kazi kwa mazoea huku akisisitiza umuhimu wa kufuata taratibu na kanuni ili kuepusha sintofahamu zinazoweza kujitokeza katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika November 27,2024.Sambamba na kauli mbiu isemayo "Serikali za Mitaa sauti ya Wananchi jitokeze kushiriki Uchaguzi".

Wito huo umetolewa leo Octoba Mosi,2024 wakati wa ufunguzi wa semina ya mafunzo kwa wasimamizi wasaidizi kwa ngazi ya Jimbo,Kata na Mtaa uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Arnatoglou Jijini Dar es Salaam.

Aidha Ndg. Mabelya ameeleza kuwa mafunzo hayo ya siku (1) yamelenga kuhakikisha kwamba uchaguzi unafanyika kwa haki na ufanisi, huku yakiwaandaa wasimamizi wasaidizi na kuwapa ujuzi wa kutosha katika kusimamia mchakato wa uchaguzi kwa kuhakikisha kwamba kila hatua inatekelezwa kwa mujibu wa sheria, Kanuni na taratibu za uchaguzi.

Aidha, Ndg.Mabelya amewataka washiriki hao kuzingatia mafunzo pamoja na kutoa uzoefu wao wa usimamizi wa siku za nyuma ili iwe rahisi katika utekelezaji wa jukumu zima la uchaguzi wa Serikali za Mitaa ifikapo Novemba 27, 2024 huku akiwakumbusha kuzingatia falsafa ya 4R (Reconciliation, Reforms, Resilience na Rebuild) ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kifanikisha zoezi hilo kwa haki na uzalendo kwa maslahi ya Jiji na Nchi kwa ujumla.

Halikadhalika, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wamekula kiapo cha uaminifu, utii ,uadilifu na kutunza siri katika kutimiza majukumu yao na kuwatendea haki watu wote kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

# MKUU WA WILAYA YA ILALA AHIMIZA VIJANA KUJIANDIKISHA KATIKA DAFTARI LA MPIGA KURA LA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA




Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo amewahimiza Vijana wenye sifa za kupiga kura kujiandikisha katika daftari la mpiga kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambalo limeanza Octoba 11 na linatarajiwa kukamilika Oktoba 20, 2024.

Mhe. Mpogole ametoa wito huo Leo Oktoba 12, 2024 mara baada ya kumaliza Zoezi la usafi katika Mitaa mbalimbali ya Kariakoo lililoandaliwa na Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) yenye lengo la kutunza mazingira na kuhamasisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa .

Akiongea na wanafunzi pamoja na Wananchi waliojitokeza kwenye zoezi hilo, Mhe. Mpogolo amesema ”Niwapongeze viongozi wa TAHLISO kwa kuona umuhimu wa kufanya usafi na kuhamasisha Uandikishaji katika daftari la mpiga kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hivyo nawasisitiza vijana mjitokeze kwa wingi kujiandikisha ili muweze kuchagua viongozi bora kwa maslahi ya Mitaa yetu na Taifa kwa ujumla, niwaombe muendelee kuwahamasisha na watu wengine katika mitaa yenu kushiriki ili kutimiza haki yao ya kikatiba ya kupiga kura ifikapo Novemba 27, 2024"

Kwa upande wake Rais wa @tahliso_official Bi. Zaynab Kitima amesema nia yao ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambae amekua kinara katika mazingira na utalii , huku akimuhakikishia Mkuu wa Wilaya ya Ilala kuendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi na wanafunzi kuendelea kujiandikisha katika daftari la mpiga kura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.
















**SHIRIKI UCHAGUZI**
**WA SERIKALI ZA MITAA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

JIANDIKISHE PIGA KURA

2024

OFISI YA RAIS TAMISEMI

**EWE MWANANCHI, JIANDAE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NOVEMBA 27, 2024.**

CITY FM RADIO
91.7 Mhz

# SIKILIZA 91.7 FM DSM

Redio inayomilikiwa na kuendeshwa chini ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini(GCU) - Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.




cityfmdsm

**91.7FM** DSM

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
S.L.P 20950
1 BARABARA YA MOROGORO
11882 DAR ES SALAAM
**SIMU:** 0738 378 386
**NUKUSHI:** 2128800
**BARUA PEPE:** info@dcc.go.tz
**TOVUTI:** www.dcc.ho.tz